## EAST AFRICAN COMMUNITY
## EAST AFRICAN LEGISLATIVE ASSEMBLY

### INTERNAL MEMO

| | | |
|---|---|---|
| **REF** | : | **EALA/MEM/11** |
| **TO** | : | Hon. Dr. James Ndahiro<br>**Chairperson, CTI Committee** |
| **CC** | : | Speaker, SG, RO |
| **FROM** | : | Clerk |
| **DATE** | : | August 27, 2010 |
| **SUBJECT** | : | **COMPLAINT BY TANZANIA BUSINESSPEOPLE DEALING IN IMPORTED CHICKEN/EGGS** |

---

Attached is a complaint from a section of Tanzania businesspeople dealing in chickens/eggs brought to the attention of the Hon. Speaker of EALA by Hon. Dr. Fortunatus L. Masha.

The Hon. Speaker hereby refers the matter to your Committee for study and advice.

**Kenneth Madete**

Enc.

WAUZA MAYAI SOKO KUU MWANZA,
C/O YUNUS ALSEN CHILONGOZI,
S.L.P 673,
MWANZA.
16 08 2010

DR .F.L MASHA (MB),
JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI.
S.L.P 1906,
MWANZA.

Kumb. WBM /SK / MZA / 36

Mheshimiwa,

**OMBI LA KUFUTA ZUIO LA KUINGIZA MAZAO YATOKANAYO NA NDEGE – MAYAI - KUKU – VIFARANGA.**

Tafadhali husika na kichwa cha habari. Tarehe 7 / 6 / 2006 Serikali ilipiga marufuku kuingiza hapa Tanzania kuku, vifaranga na mayai kutoka sehemu zote duniani. Kwa barua yenye Kumb. No BA.34/538 ya tarehe 7/6/2006.

Ni muda mrefu tangu amri hiyo itolewe bila kupitia marejeo ya athari itokanayo na amri hiyo. Sisi wafanya biashara wa mayai, vifaranga na kuku wa Mikoa ya Kanda ya Ziwa hususani Mkoa wa Mwanza tumeathirika sana na kuendelea na kuzuiwa kufanya biashara hii. Baada ya kuanzishwa SOKO HURIA sisi tulifikiri na biashara ya mayai imeruhusiwa kumbe siyo. Tunapokwenda Kampala kuchukua mayai kupitia mpaka wa Kenya na Uganda (BUSIA) tunapita bila kikwazo, lakini tukifika katika mpaka wa Kenya na Tanzania (SIRARI) tunazuiwa kuingiza mayai yanayotoka Uganda, lakini yanayotoka Kenya yanakubaliwa.

Tunapotoka Kampala tukifika mpakani (MUTUKULA) mayai yanazuiwa. Hata tukipitisha kwenye meli za mizigo kutoka Port Bell Uganda kuja Mwanza South Port mayai yanazuiwa kupakuliwa na mara nyingi meli kurudishwa na mayai hadi Port Bell Uganda. Watu wamepata hasara sana.

Mheshimiwa Mbunge wetu, cha kushangaza ni Serikali hii hii ambayo imeruhusu wafanya biashara kutoka Uganda, Kenya , Rwanda, Burundi hadi DRC kuchukua mchele kwa matani mengi sana kupeleka kwenye nchi zao na nchi zaidi za mbali kama Sudan, Chad, Somali.

Mchele huu tunashuhudia ukipakiwa kwenye meli za mizigo hapa Mwanza South Port kwa matani mengi sana. Tunakuhakikishia Mheshimiwa muda si mrefu njaa itaingia hapa nchini. Kwani mwezi June 2010 mchele tulinunua kwa Shs. 450/= kwa kilo moja sasa hivi ni Shs. 750/= kwa kilo. Sisi tunazuiwa kuleta mayai. Wakati tulipokuwa tunaingiza mayai kihalali tray moja tukiuza Shs. 3000/= sawa na yai moja sh 100/= .Sasa hivi wanaobahatika kuingiza mayai kwa magendo wanauza tray moja Tsh 7500/= sawa na yai moja Tsh 250/=. Je , wito wa Rais wa maisha bora kwa kila Mtanzania yatapatikanaje?, Hivi ni kweli Rais anayaelewa yanayotendeka ?. Tunakuomba wewe mwakilishi wetu utusaidie Mheshimiwa.

Tunatanguliza shukrani kwa msaada wako.

NI SISI WAFANYABIASHARA YA MAYAI MWANZA

1. YUNUS A. CHILONGOZI ---------------------------------- [signature]
2. FELIX FILICIAN ---------------------------------- [signature]
3. ANGELINA KAPECHE ------------ Kapeche ------------
4. NDUA MASUKE ------------ Masuke ------------
5. JULIANA KASILE ------------ Kasile ------------
6. MOHAMED RASHID ------------ Rashid ------------
7. ALLY CHIBERENGE ------------ Renge ------------
8. ASHA SHABAN ------------ Asha Shaban ------------

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**WIZARA YA MAENDELEO YA MIFUGO**

Telegrams "MIFUGO"
Telephone 255 22 2862592
Fax. 255 22-2862538
In reply please quote:

Mifugo Temeke,
S.L.P. 9152,
**DAR ES SALAAM**

9/6/06 7/6

Kumb. Na. BA.34/538

7/6/2006

## TANGAZO KWA UMMA

**YAH: KUPIGA MARUFUKU KWA MUDA UAGIZAJI NA UINGIZAJI WA KUKU, NDEGE WENGINE NA MAZAO YAKE KUTOKA NCHI ZOTE DUNIANI KUTOKANA NA TISHIO LA UGONJWA WA MAFUA MAKALI YA NDEGE**

Kwa Mamlaka niliyopewa na Sheria ya Magonjwa ya Wanyama Na. 17 ya Mwaka 2003, katika sehemu ya 54, Mimi Dkt. J.O. Mollel (BVSc. Dar), Mkurugenzi wa Huduma za Mifugo, ninaagiza kuwa uingizaji wa kuku, ndege na mazao yake kutoka **NCHI ZOTE DUNIANI** umezuiliwa kuanzia leo tarehe 7/6/2006 kutokana na tishio la Ugonjwa wa Mafua Makali ya Ndege.

Amri hii inafuta amri zote zilizotolewa awali ambazo ziliweka kizuizi kwa nchi zilizoorodheshwa kuwa zimekumbwa na virusi vya ugonjwa huo aina ya H5N1 na H5N2. Tangazo hili linahusu nchi zote duniani zilizopatwa na ambazo hazijapatwa na ugonjwa huu.

Kuanzia tarehe ya tangazo hili, uagizaji na uingizaji nchini wa kuku, vifaranga, ndege na mazao yake kutoka nchi zote duniani umepigwa marufuku mpaka hapo itakapotangazwa tena. Aidha, vibali vyote vilivyotolewa awali kabla ya tarehe iliyotajwa kwenye tangazo hili vimefutwa

Tangazo hili pia litatolewa kwenye Gazeti la Serikali.

Dkt. J.O.Mollel
**MKURUGENZI WA HUDUMA ZA MIFUGO**

**Nakala:**

- Kamishina Mkuu - Mamlaka ya Mapato Tanzania
- Inspekta Jenerali wa Polisi
- Mkurugenzi Mkuu - Mamlaka ya Chakula na Dawa
- Ukaguzi wa Mifugo na Mazao ya Mifugo -Vituo vyote vya mpakani
- Vyombo vya Habari.